# KUMKUFURU ROHO MTAKATIFU !

*Je, kuna dhambi ambayo Mungu hawezi kusamehe?*

**Shemeji Melayeki**

**Kumkufuru Roho Mtakatifu © 2025**

**Shemeji Melayeki**

**Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili bila ruhusa ya maandishi ya mwandishi isipokuwa kwa nukuu mbalimbali na matumizi ya kufundishia.**

SIMU: +255 714 548 565

Email: *shemeji.melayeki@gmail.com*
YouTube: *Shemeji Melayeki*
Instagram: *apostle_shemeji_melayeki*
Twitter: *@melayeki*
Facebook: *Ap Shemeji Melayeki*

**ISBN - 978-9912-9884-4-6**

Kimepigwa Chapa Na: **KLIMAX SOLUTIONS – ARUSHA**

**+255 658 288 054**

**+255 687 699 862**

# YALIYOMO

SHUKRANI........................................................................iii

SURA YA 1 ........................................................................ 1

*VITABU VINNE VYA INJILI* .................................................. 1

SURA YA 2 ........................................................................ 9

*NYARAKA ZA MITUME* .......................................................... 9

SURA YA 3 ........................................................................ 21

*KUMKUFURU ROHO MTAKATIFU?* .................................. 21

SURA YA 4 ........................................................................ 41

*KWA HIYO HAIWEZI KUSAMEHEWA?* ............................. 41

# SHUKRANI

Nilikwama katika namna yangu ya kufasiri Biblia hadi nilipopata mafundisho ya Mchungaji Chris Onayinka. Namna yangu ya kufasiri Biblia ilibadilika na kupokea mwanga mpya wa kuyaona maandiko matakatifu. Mafundisho na maandishi yangu yameathiriwa na namna yake yenye faida kubwa katika usahihi wa kuyasoma na kuyaelewa maandiko. Ninashukuru sana kwamba huduma yake inaendelea kunijenga na hatimaye huduma yetu.

Kwa familia yangu, mara nyingi nimekuwa macho usiku wakati wamelala, kwa utulivu mkubwa walionipa. Mke wangu Neema amekuwa msaada mkubwa katika kuhakikisha ninafanikisha uandaaji wa kitabu hiki.

Kwa timu ya watu waliojitolea kujifunza kupitia kwangu kwenye huduma ya Global Family Gatherings; wachungaji wetu na maaskofu, wamekuwa sababu ya kunifanya nijitume zaidi.

Kwa wadau wanaofanya huduma pamoja na mimi kwa njia ya sadaka zao ili kuhakikisha kazi hii haikwami, wamekuwa waaminifu kwa rasilimali zao ili kweli hii ienee zaidi.

# SURA YA 1

## *VITABU VINNE VYA INJILI*

Vitabu vinne vya injili vinaitwa ushahidi wa macho (*eye-witness account*). Ni mambo ambayo watu waliyaona na kuyashuhudia. Kwa hiyo, ni vyema kujua kuwa:-

*1.* Wewe siyo hadhira yao ya moja kwa moja (primary audience). Ijapokuwa vitakufaa wewe leo, lakini mwandishi alikuwa anaongea na watu anaowafahamu yaani Wayahudi ambao ni wanafunzi wa Yesu, waandishi/wazee, mafarisayo, masadukayo, au wengine kama vile Theofilo. Hadhira huamua aina ya lugha na uchaguzi wa maneno na hata mifano.

Angalia **Mathayo 13:3,13, 34-35, 53** *[3] Akawaambia mambo mengi kwa mifano, akisema, Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda. [13] Kwa sababu hii nasema nao kwa mifano; kwa kuwa wakitazama hawaoni, na wakisikia hawasikii, wala kuelewa. … [34]Hayo yote*

*Yesu aliwaambia makutano kwa mifano; wala pasipo mfano hakuwaambia neno; [35] ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema, Nitafumbua kinywa changu kwa mifano, Nitayatamka yaliyositirika tangu awali… [53] Ikawa Yesu alipoimaliza mifano hiyo, alitoka akaenda zake. Kukataliwa kwa Yesu katika Nazareti*

**Mathayo 21:45**

[45] *Wakuu wa makuhani na Mafarisayo, waliposikia mifano yake, walitambua ya kuwa anawanenea wao.*

**Marko 3:23** *[23] Akawaita, akawaambia kwa mifano, Awezaje Shetani kumtoa Shetani?*

**Mark 4:2,10** *[2] Akawafundisha mambo mengi kwa mifano, akawaambia katika mafundisho yake, [10] Naye alipokuwa peke yake, wale watu waliomzunguka, na wale Thenashara, walimwuliza habari za ile mifano.*

**Marko 4:11-13** [11] *Akawaambia, Ninyi mmejaliwa kuijua siri ya ufalme wa Mungu, bali kwa wale walio nje yote hufanywa kwa mifano, [12] ili wakitazama watazame, wasione; Na wakisikia wasikie, wasielewe; Wasije wakaongoka, na kusamehewa. [13] Akawaambia, Hamjui mfano huu? Basi mifano yote mtaitambuaje?*

**Marko 4:33** *[33] Kwa mifano mingi ya namna hii alikuwa akisema nao neno lake, kwa kadiri walivyoweza kulisikia.*

**Marko 12:1** [1] *Akaanza kusema nao kwa mifano; Mtu mmoja alipanda shamba la mizabibu, akazungusha ugo, akachimba shimo la shinikizo, akajenga mnara, akapangisha wakulima, akasafiri.*

**Luka 1:1-4** *Kwa kuwa watu wengi wametia mikono kutunga kwa taratibu habari za mambo yale yaliyotimizwa katikati yetu, 2 kama walivyotuhadithia wale waliokuwa mashahidi wenye kuyaona, na watumishi wa lile neno tokea mwanzo, 3 nimeona vema mimi nami, kwa kuwa nimejitafutia usahihi wa mambo hayo yote tangu mwanzo, kukuandikia kwa taratibu, Theofilo mtukufu, 4 upate kujua hakika ya mambo yale uliyofundishwa.*

**Luka 8:10** *[10] Akasema, Ninyi mmepewa kuzijua siri za ufalme wa Mungu; bali wengine kwa mifano, ili wakiona wasione, na wakisikia wasielewe.*

Kwa hiyo, waliokuwa wanaandikiwa walikuwa wanajua kwa hakika kwa nini mifano ya aina hiyo ilichaguliwa. Hebu fikiria mtu atoe mfano wa kilimo cha matikitiki maji jangwani au ufugaji wa ngamia kwenye sehemu za mvua tele. Ni dhahiri kwamba, haiwezekani.

2. Sehemu kubwa ya vitabu hivyo zinazungumzia ahadi-zilitimia katika ufufuo wa Yesu Kristo. Sura za mwisho zinaonyesha hayo;

**Luka 24:44** *[44] Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja*

*nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.*

Angalia Kleopa namwenzake walivyotafsiri kufa na kufufuka kwake. **Luka 24:13-32** *[13] Na tazama, siku ile ile watu wawili miongoni mwao walikuwa wakienda kijiji kimoja, jina lake Emau, kilichokuwa mbali na Yerusalemu kama mwendo wa saa mbili. [14]Nao walikuwa wakizungumza wao kwa wao habari za mambo hayo yote yaliyotukia. [15] Ikawa katika kuzungumza na kuulizana kwao, Yesu mwenyewe alikaribia, akaandamana nao. [16] Macho yao yakafumbwa wasimtambue. [17] Akawaambia, Ni maneno gani haya mnayosemezana hivi mnapotembea? Wakasimama wamekunja nyuso zao. [18] Akajibu mmoja wao, jina lake Kleopa, akamwambia, Je! Wewe peke yako u mgeni katika Yerusalemu, hata huyajui yaliyotukia humo siku hizi? [19] Akawauliza, Mambo gani? Wakamwambia, Mambo ya Yesu wa Nazareti, aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote; [20] tena jinsi wakuu wa makuhani na wakubwa wetu walivyomtia katika hukumu ya kufa, wakamsulibisha. [21] Nasi tulikuwa tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli. Zaidi ya hayo yote, leo ni siku ya tatu tangu yalipotendeka mambo hayo; [22] tena, wanawake kadha wa kadha wa kwetu walitushitusha, waliokwenda kaburini asubuhi na mapema, [23] wasiuone mwili wake; wakaja wakasema ya kwamba*

*wametokewa na malaika waliosema kwamba yu hai. [24] Na wengine waliokuwa pamoja nasi walikwenda kaburini wakaona vivyo hivyo kama wale wanawake walivyosema, ila yeye hawakumwona. [25] Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii! [26] Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake? [27] Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.[28] Wakakikaribia kile kijiji walichokuwa wakienda, naye alifanya kama anataka kuendelea mbele. [29] Wakamshawishi wakisema, Kaa pamoja nasi, kwa kuwa kumekuchwa, na mchana unakwisha. Akaingia ndani kukaa nao. [30] Ikawa alipokuwa ameketi nao chakulani, alitwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa. [31] Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua; kisha akatoweka mbele yao. [32] Wakaambiana, Je! Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia maandiko?*

Umeona Yesu alivyotafsiri? *[25] Akawaambia,* ***Enyi msiofahamu,*** *wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii! [26] Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake? [27] Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.*

3. Ufunuo haukuandikwa kwenye vitabu hivyo vinne yaani inaonekana na kusikitisha kwa Yesu anateswa, kufa na hatimaye kufufuka. Na bado walikuwa wanasikitika kuwa hayupo kaburini. Hivyo inaonekana wazi Yesu alikuwa anaongewa na watu waliokuwa hawaelewi. (rudia kisa cha Kleopa na mwenzake).

Anaonekana kama anateswa mwenyewe…

Ufunuo kwenye nyaraka ni kwamba- TULISULIBIWA pamoja naye, TUKAFA pamoja naye, tukazikwa pamoja naye na tukafufuka pamoja naye.

**Waefeso 2:4-6** *[4] Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; [5] hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema. [6] Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu;*

Angalia *alituhuisha pamoja na Kristo; Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho…*

**Wakolosai 2:20** *[20] Basi ikiwa mlikufa pamoja na Kristo mkayaacha yale mafundisho ya awali ya ulimwengu, kwa nini kujitia chini ya amri, kama wenye kuishi duniani.*

Angalia *mlikufa pamoja na Kristo*. Huwezi kuona haya maneno kwenye Mathayo, Marko, Luka na Yohana.

**Warumi 6:8** *[8] Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye.*

Angalia … tulikufa pamoja na Kristo…tutaishi pamoja naye.

**Wagalatia 2:20** *[20] Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.*

Pia hapa… *Nimesulibiwa pamoja na Kristo… Kristo yu hai ndani yangu…*

**Wakolosai 3:1, 3** *[1] Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. [3] Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu.*

Angalia tena, *mmefufuliwa pamoja na Kristo* …

Kwenye vitabu vine vya injili inaonekana anateswa mwenyewe, anasulubiwa mwenyewe, anakufa mwenyewe, anazikwa mwenyewe, na anafufuka mwenyewe.

Kwa hiyo tunatumia nyaraka kupima fundisho kwenye vitabu vinne vya injili- PIA nyaraka ziliandikwa kimsingi kwa ajili ya KANISA-WAAMINI tofauti na vitabu vinne

(Mathayo-Yohana) ambapo hata mazungumzo ya wasioamini pia yamerekodiwa.

KWA HIYO, FUNDISHO LOLOTE KWENYE VITABU VINNE VYA INJILI, TUTAANGALIA KAMA LILIHUBIRIWA KWENYE MATENDO YA MITUME NA MSISITIZO WA FUNDISHO HILO KWENYE NYARAKA ZA MITUME.

Je, nyaraka za mitume zinafundisha kuwa kuna dhambi Mungu hawezi kusamehe?

Pia, inaonekana wazi kuwa Yesu hakuwafundisha kila kitu kwenye vitabu vya Injili.

Twende sasa tukaliangalie hilo katika sura inayofuata.

# SURA YA 2

## *NYARAKA ZA MITUME*

Tuanze na maneno ambayo Yesu ambayo aliyasema kwa wanafunzi wake alipofufuka kutoka kwa wafu.

**Luka 24:25** *[25] Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii!*

Maneno haya "*yote waliyoyasema manabii*" ni lazima yaelezewe kwenye muktadha.

Angalia **Luke 24:26-27** *[26] Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake? [27] Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo* ***yaliyomhusu yeye mwenyewe.***

Yesu kusema… "*yote waliyoyasema manabii*" hakuwa anazungumzia KILA kitu walichosema manabii bali "*mambo* ***yaliyomhusu yeye mwenyewe.*** - yaani kupata mateso na kuingia katika utukufu wake. Kwa hiyo mambo yaliyomhusu ambayo manabii waliyasema ni Yesu kupata mateso na kuingia katika utukufu wake. Petro pia alizungumzia hilo kwenye waraka wake wa kwanza...

Angalia **1 Petro 1:10-11** *[10] Katika habari ya **wokovu** huo **<u>manabii</u>** walitafuta-tafuta na kuchunguza-chunguza, ambao walitabiri habari za neema itakayowafikia ninyi. [11] Wakatafuta ni wakati upi, na wakati wa namna gani ulioonywa na Roho wa Kristo aliyekuwa ndani yao, ambaye alitangulia <u>kuyashuhudia</u> **mateso yatakayompata Kristo, na utukufu utakaokuwako baada ya hayo**.*

Kwenye waraka wake wa Pili pia alisema vile vile.
**2 Petro 1:19-20** *[19] Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'aayo mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu. [20] Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu.*
Petro anazungumzia unabii katika Maandiko matakatifu kwamba ni unahusu ***mateso yatakayompata Kristo, na utukufu utakaokuwako baada ya hayo***.

Angalia Paulo alivyowaambia kanisa la Rumi. Angalia **Warumi 1:1-4** *[1] Paulo, mtumwa wa Kristo Yesu, aliyeitwa kuwa mtume, na kutengwa aihubiri **Injili** ya Mungu; [2] ambayo Mungu amekwisha kuiahidi kwa kinywa cha manabii wake katika maandiko matakatifu; [3] **yaani, habari za Mwanawe**, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili, [4] na **kudhihirishwa** kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya*

*utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu…*

Neno *kudhihirishwa* au "***declared***" kwa Kingereza cha KJV lilitafsiriwa kwenye neno la Kigiriki "**horizo**". Ikiwa na maana ya kutambulishwa, kuonyeshwa.

Ukisoma maneno haya ya Paulo anamaanisha kuwa unaposoma habari za manabii kwa hapa akimaanisha Mwanzo mpaka Malaki, lazima ujue namna ya kuona au kutambua Injili ambayo ni habari za Mwana wa Mungu - Yesu Kristo. Ukisoma hapo utaiona kama ahadi ambayo imedhihirishwa au kuwekwa wazi katika ufufuo wa Kristo.

Kile ambacho Paulo anakihubiri na kuandika kwenye nyaraka zake anazitoa Mwanzo mpaka Malaki.

Kwa hiyo barua zake ni maelezo ya kiuchambuzi ya Mwanzo mpaka Malaki. Ndiyo maana Paulo anaviita vitabu vya Agano la Kale (Maandiko) kuwa ni "siri".

Angalia kwenye **Warumi 16:25-26** *[25] Sasa na atukuzwe yeye awezaye kuwafanya imara, sawasawa na injili yangu na kwa kuhubiriwa kwake Yesu Kristo, sawasawa na ufunuo wa ile siri iliyositirika tangu zamani za milele, [26] ikadhihirishwa wakati huu kwa maandiko ya manabii, ikajulikana na mataifa yote kama alivyoamuru Mungu wa milele, ili waitii Imani*:

Angalia maneno ***ufunuo wa ile siri*** *...*

Angalia pia **Waefeso 3:3-4,9** *[3] ya kwamba kwa kufunuliwa nalijulishwa siri hiyo, kama nilivyotangulia kuandika kwa maneno machache. [4] Kwa hayo, myasomapo, mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika*

*siri yake Kristo....[9] na kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote;*
Paulo anasema wakisoma nyaraka zake wanaweza *kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo.*

Kwenye waraka wake kwa **Wakolosai 1:26** *[26] siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake;*
Neno **"siri"** au kwa Kingereza cha KJV **"mysteries"** limetafsiriwa kutoka kwenye neno la Kigiriki "**musterion**", likiwa na maana *jambo ambalo linahitaji kuelezewa au kufunuliwa.* Haina maana ya jambo lililofichwa ili watu wasijue kama ambavyo tumezoea kutumia neno **siri** namna hiyo. Mungu hana haja ya kuficha vitu ili watu wasijue. Kwa hiyo ufunuo wa hiyo siri ndiyo nyaraka za mitume yaani Paulo na wenzake.
Angalia tena **Waefeso 3:3-4** *[3] ya kwamba kwa kufunuliwa nalijulishwa siri hiyo, kama nilivyotangulia kuandika kwa maneno machache. [4] Kwa hayo, myasomapo, mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo.*
Kwa maneno mengine, ni sawa kabisa tukisema, ni ufunuo wa wazi wa yale yaliyoko kwenye Maandiko Matakatifu yaani Mwanzo mpaka Malaki.

Turudi tena **Waefeso 3:2-5** *[2] ikiwa mmesikia habari ya uwakili wa neema ya Mungu niliyopewa kwa ajili yenu; [3] ya kwamba kwa kufunuliwa nalijulishwa siri hiyo,*

*kama nilivyotangulia kuandika kwa maneno machache. [4] Kwa hayo, myasomapo, mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo. [5] Siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine; kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi katika Roho*;

Neno *myasomapo au* **'read'** kwa Kingereza cha KJV ni neno la Kigiriki "**anaginosko**". Ni kitendo au kitenzi. Limetokana na maneno mawili ya Kigiriki:

**ANA** maana yake ni kurudia rudia, kuwa makini.

**GINOSKO** maana yake ni kufahamu, kujua.

**"ana"** kurudia rudia, kuwa umakini, kuchukua yote/vyote.

**"Ginosko"** kufahamu, kujua;

Kwa hiyo Paulo anaposema *myasomapo* "**anaginosko**" hamaanishi usomaji tu wa kawaida, wala huku si kusoma kwa kukariri tu na wala si kusoma ili kumaliza bali ni kusoma ili kuelewa. Ni kusoma kwa umakini kabisa na kwa kurudiarudia. Katika kujenga ufahamu thabiti, huwezi kukwepa kurudiarudia.

Ndiyo maana kanuni bora kabisa kuhusu kuelewa Biblia kwanza ni **kusoma tu, tena kusoma vizuri.**

Kwa hiyo ukisoma nyaraka kwa umakini utaona namna gani Paulo na mitume wengine walisoma Maandiko Matakatifu au Agano la Kale na kuja na ufunuo wa hiyo siri.

Hii ni sawa na kusema, ukisoma vizuri nyaraka za mitume; utakutana na vitu viwili:

1. Fundisho au ujumbe ambao wanawasilisha kwa wasomaji, na
2. Mtindo (***pattern***) ambao unaweza kuufuata na kupata kile walichokipata na kuandika kwenye nyaraka zao.

**Tofuati ya nyaraka na vitabu vinne vya injili**!

Tuangalie maneno ya Yesu kwa wanafunzi wake...
**Yohana 16:12-15** *[12] Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa. [13] Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. [14] Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari.*
*[15] Na yote aliyo nayo Baba ni yangu; kwa hiyo nalisema ya kwamba atatwaa katika yaliyo yangu, na kuwapasheni habari.*
Neno *kuyastahimili* au kwa Kingereza cha KJV "**bear**" limetafsiriwa kutoka kwenye neno la Kigiriki **bastazō̄** lenye maana ya kuchukua kitu ili kubeba, kuvumilia au kuweza kukaa nacho vyema. Kwa hiyo Yesu alimaanisha nini? Yesu kusema *nikali ninayo mengi ya kuwaambia* ina maana kuna mambo aliacha kufundisha siyo kwa sababu hakuyajua au hakuweza kufundisha ila ni kwa sababu watu waliomzunguka wasingeweza kubeba au kuelewa.
Angalia maelezo yake baada ya kusema hivyo kwenye mstari wa 13…

**Yohana 16:13** *[13] Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.*
Neno **atawapasha** ni neno la Kigiriki "**anaggello**", lenye maana ya kuona jambo na kulitangaza. Kwa hiyo huyo Roho wa kweli atawafunulia mambo yajayo.
Je, Yesu alikuwa anamaanisha ufunuo gani? Ni kitu gani atawafunulia? Ni ufunuo wa mtu binafsi, kwamba Roho wa kweli atamfunulia KILA mtu kitu chake maalumu?
Tuangalie hilo. Mstari wa **14** na **15 unatupa majibu.**
**Yohana 16:14-15** *[14] Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari. [15] Na yote aliyo nayo Baba ni yangu; kwa hiyo nalisema ya kwamba atatwaa katika yaliyo yangu, na kuwapasheni habari*.
Anasema ***atanitukuza mimi...atatwaa katika yaliyo yangu... ambayo ni ya Baba.*** Umeona ya kuwa huu siyo ufunuo binafsi? Mara nyingi tumesoma mstari wa 12 na 13 kumaanisha kuwa kuna mambo ambayo Yesu hakuyasema ambayo [sisi] tutafunuliwa na Roho Mtakatifu. Wakati mwingine tunadiriki hata kusema "USIFUNGWE NA BIBLIA -ROHO MTAKATIFU ATATUONYESHA MAMBO AMBAYO HAYAKO KWENYE BIBLIA" Hii ni ajabu sana, huku ni kujikwaa kabisa, maana Yesu alikuwa anazungumzia jambo lingine kabisa. Mstari wowote kwenye Biblia ukichukuliwa nje ya muktadha huleta majanga makuu. Anasema

*atanitukuza mimi... atatwaa katika yaliyo yangu... ambayo ni ya Baba.* Rahisi tu.
Anaendelea mstari wa 16… **Yohana 16:16** *[16] Bado kitambo kidogo nanyi hamnioni; na tena bado kitambo kidogo nanyi mtaniona.*
Angalia anavyosema... kitambo kidogo **haonekani**, kitambo kidogo **ataonekana**. Ina maana hataonekana na atarudi…
Mstari wa 10 anasema anaenda wapi?
**Yohana 16:10** *[10] kwa habari ya haki, kwa sababu mimi naenda zangu kwa Baba, wala hamnioni tena;*
Yesu alimaanisha nini kusema *"naenda zangu kwa Baba?"*
Tuangalie… **Yohana 20:17** *[17] Yesu akamwambia. Usinishike; kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba. Lakini enenda kwa ndugu zangu ukawaambie, Ninapaa kwenda kwa Baba yangu naye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu.*
Kwa hiyo mbele ametaja... Kupaa kwake... Ndiyo kwenda kwa Baba.
Kwa hiyo aliposema *atanitukuza... mambo yajayo... atayatwaa katika yaliyo yangu...* kwenye **Yohana 16:12-15**, alikuwa anazungumzia habari za kufa kwake, kuzikwa ufufuo na kupaa kwake kwa Baba. Hiyo ni sawa na kile ambacho Luka aliandika… *habari za mateso ya Kristo na utukufu utakaofuata*…ndicho ambacho wanafunzi wake walikuwa hawaelewi kabisa.
Alipofufuka wanafunzi wake walikuwa wanaongea kama watu wasioamini. Angalia alivyowaambia

**Luka 24:25-27** *[25] Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye* ***mioyo mizito ya kuamini*** *yote waliyoyasema manabii! [26] Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake?[27] Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote* ***mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.***

Angalia tena hapa, **Luka 24:36-47** *[36] Na walipokuwa katika kusema habari hiyo, yeye mwenyewe alisimama katikati yao, akawaambia, Amani iwe kwenu. [37] Wakashituka, wakaogopa sana, wakidhani ya kwamba wanaona roho. [38] Akawaambia, Mbona mnafadhaika? Na kwa nini mnaona shaka mioyoni mwenu? [39] Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo. [40] Na baada ya kusema hayo aliwaonyesha mikono yake na miguu yake. [41] Basi walipokuwa* ***hawajaamini kwa furaha, huku wakistaajabu,*** *aliwaambia, Mna chakula cho chote hapa? [42] Wakampa kipande cha samaki wa kuokwa. [43] Akakitwaa, akala mbele yao. [44] Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi. [45]* ***Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko.*** *[46] Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; [47] na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa*

*jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.*
Kwa hiyo, baada ya ufufuo wa Yesu Kristo, akili zao zilielewa.
Kusema **"Roho wa kweli atawafunulia mambo yajayo"** hakuwa anazungumzia ufunuo binafsi wa kipekee kwa kila mtu, bali uelewa wa Maandiko Matakatifu juu ya ahadi ya Baba kupitia manabii ambayo ilikuja kutimizwa katika ufufuo wa Yesu Kristo kutoka kwa wafu. Na hili lilikuwa ni ujumbe wa moja kwa moja kwa wanafunzi wake. Wanafunzi wake **walifunuliwa na walielewa baada ya ufufuo.**
Ndiyo maana Paulo alisema kwa kanisa la Korintho, **1 Wakorintho 2:6-10** *[6] Walakini iko hekima tusemayo kati ya wakamilifu; ila si hekima ya dunia hii, wala ya hao wanaoitawala dunia hii, wanaobatilika; [7] bali twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu; [8] ambayo wenye kuitawala dunia hii hawaijui hata mmoja; maana kama wangaliijua, wasingalimsulibisha Bwana wa utukufu; [9] lakini, **kama ilivyoandikwa**, Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. [10] Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu*.
Paulo anasema **kama ilivyoandikwa** anaonyesha kuwa alikuwa ananukuu Maandiko Matakatifu yaani Mwanzo

mpaka Malaki. Kimaalumu kabisa, Paulo alikuwa ananukuu kitabu cha nabii Isaya...

Angalia **Isaya 64:4** *[4] Maana tangu zamani za kale watu hawakusikia, wala kufahamu kwa masikio, wala jicho halikuona Mungu, ila wewe, atendaye mambo kwa ajili yake amngojaye.*

Ilikuwa imeandikwa kwenye Maandiko Matakatifu, hawakuelewa. Yesu pia alitumia maneno hayo kama ambavyo Mathayo ameandika...

**Mathayo 13:17** *[17] Kwa maana, amin, nawaambia, Manabii wengi na wenye haki walitamani kuyaona mnayoyaona ninyi, wasiyaone; na kuyasikia mnayoyasikia ninyi, wasiyasikie.*

Ukirudi kwenye 1 Wakorintho 2, kwenye mstari wa **7** anasema twainena **hekima ya Mungu katika siri… wisdom of God in a mystery** na mstari wa **10** anasema **Mungu ametufunulia sisi kwa Roho wake.**

Swali la msingi: Mungu amewafunulia nini kwa Roho wake?

Rudi **1 Wakorintho 2:16** *[16] Maana, Ni nani aliyeifahamu nia ya Bwana, amwelimishe? Lakini sisi tunayo nia ya Kristo.*

Hapa pia Paulo hakuwa anazungumzia ufunuo binafsi bali ufunuo wa Kristo. Tena siyo yeye peke yake amefunuliwa, **Mungu ametufunulia sisi kwa Roho wake.**

Swali lingine, Paulo anaposema "**sisi"**, kwenye mstari wa **10** na anaposema **"twayanena"** kwenye mstari wa **13,** hawa ni akina nani?

Hii siyo mara ya kwanza Paulo amesema kuwa amefunuliwa au wamefunuliwa siri. Angalia kwenye waraka aliouandika kwenye kanisa la Efeso.

**Waefeso 3:3-5** *[3] ya kwamba kwa kufunuliwa nalijulishwa siri hiyo, kama nilivyotangulia kuandika kwa maneno machache. [4] Kwa hayo, myasomapo, mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo. [5] Siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine; kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi katika Roho;*

Kwenye mstari wa **3:** Paulo anaziita nyaraka zake, ni ufunuo wa siri (Maandiko Matakatifu) ameandika kwa maneno machache.

Kwenye mstari wa **5**: anasema wamefunuliwa Mitume wake watakatifu na manabii.

Kwa hiyo, hao akina "**sisi"** kwenye **1 Wakorintho 2:10 & 13**) ni Mitume**!** Kwa hiyo, ufunuo wa Roho ambao Paulo alikuwa anazungumzia ni nyaraka za mitume wa Kristo.

Ni sawa kabisa tukisema nyaraka (barua za mitume) ni ufunuo wa Maandiko yaani Mwanzo mpaka Malaki. Nyaraka za mitume hasa hasa nyaraka za mtume Paulo, ni ufunuo wa Kristo. Tunaweza kusema nyaraka hizi zinafunua kwa undani kile ambacho Yesu hakuyasema kwa wanafunzi wake. Kwa sababu hiyo, nyaraka ni ufunuo wa Roho, nyaraka ndiyo kweli yote.

Nyaraka ni ufunuo wa mpango wa Mungu ulioandikwa Mwanzo mpaka Malaki.

# SURA YA 3

## *KUMKUFURU ROHO MTAKATIFU?*

Kuna wimbi kubwa la mashaka kuhusu kumkufuru Roho Mtakatifu. Wengine wameambiwa ukishakufuru imetoka hiyo. Sahau kuhusu kwenda mbinguni. Sahau kuhusu uzima wa milele. Hapo unakuwa umegawiwa bure Jehanamu wala huwezi kukukuruka hata ulie machozi ya damu. Wengine wameamua kuwa wahuni maana hakuna tumaini tena. Hakuna namna. Wameacha kwenda kanisani. Wameacha kusoma Biblia. Wameacha mambo ya imani. Kwa sababu waliambiwa wameshakufuru.

Lakini wengine wamebaki na jakamoyo. Wako kanisani lakini hawana uhakika na chochote. Hawana uhakika kama wameokoka au wanawasindikiza waliookoka ambao hawajawahi kukufuru.

Hii mara nyingi huanzia kwenye maneno yaliyoandikwa kwenye **Mathayo 12:31-32** *[31]Kwa sababu hiyo nawaambia, Kila dhambi na kila neno la kufuru watasamehewa wanadamu, ila kwa kumkufuru Roho*

*hawatasamehewa. [32]Naye mtu ye yote atakayenena neno juu ya Mwana wa Adamu atasamehewa, bali yeye atakayenena neno juu ya Roho Mtakatifu hatasamehewa katika ulimwengu wa sasa, wala katika ule ujao.*

Maneno haya yamerudiwa pia na Marko kwenye **Marko 3:28-30** *[28]Amin, nawaambia, Dhambi zote watasamehewa wanadamu, na kufuru zao watakazokufuru zote; [29]bali mtu atakayemkufuru Roho Mtakatifu hana msamaha hata milele; ila atakuwa ana dhambi ya milele, [30]kwa vile walivyosema, Ana pepo mchafu.*

Luka pia hakuacha. Angalia Luka **12:10** *[10]Na kila mtu atakayenena neno juu ya Mwana wa Adamu atasamehewa, bali aliyemkufuru Roho Mtakatifu hatasamehewa.*

Yohana pekee ndiye ambaye hakuandika tukio hilo.

Lakini maandiko Matakatifu yasemaje? Kuna dhambi ambayo Mungu hawezi kuisamehe? Mtu anakuwaje na dhambi? Au anaondolewaje dhambi na kufanyika mwenye haki?

Haya ni maswali ya msingi sana kabla hatujaenda mbali.

Isaya anatabiri kwenye **Isaya 43:25** *[25]Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako.*

Anafuta kwa ajili yake MWENYEWE.

Kwenye **Zaburi 103:12** *[12]Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi.*

Hii ni sawa na kusema AMEONDOA kabisa.. maana Mashariki na Magharibi hazitakaa zikutane..

Kwenye kwenye Isaya 43:25 kasema HATAZIKUMBUKA.

Angalia mwandishi wa kitabu cha Waebrania anasema katika **Waebrania 8:10,12**

*[10]Maana hili ndilo agano nitakaloagana na nyumba ya Israeli, Baada ya siku zile, asema Bwana; Nitawapa sheria zangu katika nia zao, Na katika mioyo yao nitaziandika; Nami nitakuwa Mungu kwao, Nao watakuwa watu wangu. [12]Kwa sababu nitawasamehe maovu yao, Na dhambi zao SITAZIKUMBUKA TENA.*

AMEWEKA AGANO AMBALO NDANI YAKE HAKUNA KUMBUKUMBUKU LA DHAMBI. Mungu kutokumbuka haina maana ana ugonjwa wa kusahau ila maana yake HATAKUTENDEA KAMA VILE UMEWAHI KUKOSEA. ***He will treat you like you have never made a mistake.***

Mwandishi wa kitabu cha Waraka kwa Waebrania alikuwa ananukuu ahadi hiyo kwenye kitabu cha Nabii **Yeremia 31:31-34.** [31]*Angalia, siku zinakuja, asema Bwana, nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli,*

*na nyumba ya Yuda. [32] Si kwa mfano wa agano lile nililolifanya na baba zao, katika siku ile nilipowashika mkono, ili kuwatoa katika nchi ya Misri; ambalo agano langu hilo walilivunja, ingawa nalikuwa mume kwao, asema Bwana. [33] Bali agano hili ndilo nitakalofanya na nyumba ya Israeli, baada ya siku zile, asema Bwana; Nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. [34] Wala hawatamfundisha kila mtu jirani yake, na kila mtu ndugu yake, wakisema, Mjue Bwana; kwa maana watanijua wote, tangu mtu aliye mdogo miongoni mwao hata aliye mkubwa miongoni mwao, asema Bwana; maana nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena.*

Kwenye **Mathayo 26:28** *[28]kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi.*

Kigezo cha Ondoleo la dhambi ni mauti ya Yesu Kristo.

**Luka 24:46-47** *[46]Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;* [47]na *kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.*

Kufa na KUFUFUKA kwake ndiko kunaloleta ONDOLEO la dhambi.

**Matendo ya Mitume 2:38** *[38]Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo,*

*mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*

Kufa na KUFUFUKA ndiyo jina pale (jina siyo herufi ni **Brand/accomplishment).**

**Matendo ya Mitume 10:43** *[43]Huyo manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi.*

Manabii kwa maana ya Waandishi wa Mwanzo mpaka Malaki walitabiri hilo.

UKIMWAMINI YESU (KUFA NA KUFUFUKA KWAKE) UNAPATA ONDOLEO LA DHAMBI.

Neno KUONDOA (REMISSION) na MSAMAHA (FORGIVENESS) maana moja kwa lugha ya Kigiriki.

Neno hilo ni "**APHESIS**" angalia hapa. **Wakolosai 1:13-14** *[13]Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake; [14]ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi.*

Ndani yake Kristo TUNAO (UNAMILIKI KAMA MALI YAKO HALALI) MSAMAHA (**APHESIS**) WA DHAMBI.

**Waefeso 1:7** *[7]Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.*

Ndani yake Kristo tunao Ukombozi yaani masamaha "**aphesis**"

Neno aphesis linamaanisha KUONDOLEWA KATIKA VIFUNGO (HAPA NI DHAMBI) KWA KULIPIWA GHARAMA.

Hivyo inakuwa Bill Cleared. Kwa KUAMINI TU!. FULL STOP. Unapoamini unahamishiwa NDANI YA KRISTO yaani unakuwa umeondolewa gizani MAZIMA.

Kwanza  Yesu amefanya mara moja na akamaliza kazi yake. Angalia **Waebrania 7:27** *[27]ambaye hana haja kila siku, mfano wa wale makuhani wakuu wengine, kwanza kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe, kisha kwa ajili ya dhambi za hao watu; maana yeye alifanya hivi MARA MOJA, alipojitoa nafsi yake*.

**Waebrania 10:10** *[10]Katika mapenzi hayo mmepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo MARA MOJA tu.*

**Waebrania 9:28** *[28]kadhalika Kristo naye, akiisha KUTOLEWA sadaka MARA MOJA AZICHUKUE DHAMBI za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu.*

Angali haya maneno. MARA MOJA.  Yesu hafi kila siku. Amemaliza na amemaliza.

Mtu anaamini pia MARA MOJA DHAMBI ZAKE ZINAKUWA ZIMEONDOLEWA MILELE.

Alipoingia MARA MOJA alichukua UKOMBOZI WA MILELE. Muda gani? MILELE. MILELE NI MILELE SIYO YA MUDA AU ITAKAYO EXPIRE KESHO.

**Waebrania 9:12** *[12]wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata UKOMBOZI WA MILELE.*

Yesu ni zaidi ya DHABIHU za MIFUGO. Zilikuwa zinatolewa kila mwaka. Kwa nini?

**Waebrania 10:1-4** *[1]Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wo wote kuwakamilisha wakaribiao. [2]Kama ndivyo, je! Dhabihu hazingekoma kutolewa; kwa maana waabuduo, wakiisha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi? [3]Lakini katika dhabihu hizo liko kumbukumbu la dhambi kila mwaka. [4]Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi.*

HAIWEZI KUWAKAMILISHA, WALIJIONA BADO WENYE DHAMBI, KULIKUWA NA KUMBUKUMBUKU LA DHAMBI, HAIWEZEKANI DHABIHU HIZO ZIKAONDOA DHAMBI.

Ila Kristo ni Tofauti.

UTAKASO/UKOMBOZI kwa njia ya Yesu Kristo ni MARA MOJA ila nguvu yake inadumu MILELE.

**Waebrania 10:1-4,14** *[1]Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wo wote kuwakamilisha wakaribiao. [2]Kama ndivyo, je! Dhabihu hazingekoma kutolewa; kwa maana waabuduo, wakiisha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi? [3]Lakini katika dhabihu hizo liko kumbukumbu la dhambi kila mwaka. [4]Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi…*

*[14]Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.*

TOLEO MOJA. Utakaso wa MILELE. Siyo KUJITAKASA wanatakaswa MILELE. MARA MOJA.

Dhabihu ya Yesu ni bora zaidi ya wanyama waliotolewa kama iagizavyo torati. Walikuwa ni kivuli tu. Yesu ndiye sura yenyewe.

**Waebrania 9:12** *[12]WALA si kwa damu ya MBUZI na NDAMA, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha KUPATA UKOMBOZI WATU MILELE.*

Kwenye **Waebrania 5:8-9** *[8]na, ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata; [9]naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii.*

Anauita WOKOVU WA MILELE.

Wanaomtii maana yake WANAOMWAMINI.

Huwezi kuondoa au kufuta kitu cha MILELE.

*You cannot in anyway at any time cancel an ETERNAL REDEMPTION/SALVATION.*

Baada ya kuona hakikisho la WOKOVU, kwamba dhabihu ya Yesu ni dhabihu bora zaidi, nguvu yake ya utakaso inadumu milele ijaokuwa ilitolewa mara moja. Na mtu hupokea huu WOKOVU huo wa milele mara moja na anadumu kuwa ameokolewa MILELE.

Yesu Kristo Bwana wetu mwenyewe alitaja habari za umilele kwenye uzima tunaopewa tunapoamini. Angalia alichosema..

**Yohana 3:16** *[16]Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*

Ni uzima wa MILELE. Yaani kitu kisichoondoka ni PERMANENT siyo temporary.

Angalia Yohana anavyonukuu tena maneno ya Bwana Yesu kwenye **Yohana 10:28-29** *[28]Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu. [29]Baba yangu aliyenipa hao ni mkuu kuliko wote; wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu.*

Angalia haya maneno;

Uzima wa MILELE

Hawatapotea KAMWE

HAKUNA awezaye kuwapokonya

Baba yangu ni mkuu kuliko WOTE

Hapo unagundua hii kazi ni nguvu za Mungu (all God's power caused SALVATION).. na hakuna nguvu zenye nguvu kama nguvu za Mungu. Ukishapokea haipokonyeki. Huo ni uhakika. "VERY ABSOLUTE"

Kwenye Yohana 3, Yesu alikuwa anaongea na Nikodemo na alihusisha uzima wa MILELE na kuzaliwa mara ya pili au kuzaliwa kwa Roho.

Angalia huu mtiririko **Yohana 3:3,5-6,14-16**

*[3]Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu…*

*[5]Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu. [6]Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho…*

*[14]Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; [15]ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye. [16]Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili*

*kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*

Angalia..

Kuzaliwa mara ya pili..

Kuzaliwa kwa Roho..

Uzima wa MILELE..

(Ni kitu kimoja).

Uzima wa milele (ETERNAL life) ni maisha ya Mungu ndani ya mtu. Maisha ya MILELE.

Kuhusu Roho Mtakatifu anasema (Yohana ananukuu tena).. **Yohana 7:37-39** *[37]Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu akasimama, akapaza sauti yake akisema, Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe. [38]Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. [39]Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa.*

Roho anatolewa baada ya Yesu kutukuzwa..

Angalia anatukuzwa namna gani? **Luka 24:25-27** *[25]Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii! [26]Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake? [27]Akaanza kutoka Musa na manabii*

*wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.*

Kuingia katika UTUKUFU WAKE ni sawa na kusema ATATUKUZWA.

Kwenye muktadha walikuwa wanajadili kufa na KUFUFUKA kwake. Kitu ambacho Kleopa na mwenzake hawakuamini.

Anasema habari hiyo mbele ya wanafunzi wake wengine habari ile ile…

**Luka 24:44,46-47** *[44]Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.*

*[46]Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; [47]na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.*

Angalia vizuri. Musa na manabii waliandika juu ya KRISTO KUPATA MATESO NA KUINGIA KATIKA UTUKUFU WAKE. Anarudia habari hiyo kwa kuacha neno kutukuzwa kisha anasema KRISTO ATATESWA NA KUFUFUKA SIKU YA TATU.

Kwa hiyo ni kitu kimoja!.

Mpaka hapa Roho Mtakatifu anatolewa kwao baada ya Yesu Kristo KUFUFUKA.. sasa walimkufuruje?

Turudi kwenye muktadha mahali habari hii imeandikwa yaani **Mathayo 12:31-32** *[31]Kwa sababu hiyo nawaambia, Kila dhambi na kila neno la kufuru watasamehewa wanadamu, ila kwa kumkufuru Roho hawatasamehewa. [32]Naye mtu ye yote atakayenena neno juu ya Mwana wa Adamu atasamehewa, bali yeye atakayenena neno juu ya Roho Mtakatifu hatasamehewa katika ulimwengu wa sasa, wala katika ule ujao.*

Neno KUMKUFURU ni neno la Kingereza **blasphemy** wakati Kigiriki (lugha ya asili ya Biblia) wametumia **blasphēmia** au **blasphēmos** wakiwa na maana ya kusema vibaya/kwa uovu (evil speaking) au kutukana.

Habari yenyewe ilikuwa ni nini? Angalia **Mathayo 12:22-27** *[22]Wakati ule akaletewa mtu mwenye pepo, kipofu, naye ni bubu; akamponya, hata yule bubu akanena na kuona. [23]Makutano wote wakashangaa, wakasema, Huyu siye mwana wa Daudi?[24]Lakini Mafarisayo waliposikia, walisema, Huyu hatoi pepo, ila kwa Beelzebuli mkuu wa pepo. [25]Basi Yesu akijua mawazo yao, akawaambia, Kila ufalme ukifitinika juu ya nafsi yake, hufanyika ukiwa; tena mji au nyumba yo yote ikifitinika juu ya nafsi yake, haitasimama. [26]Na Shetani akimtoa Shetani, amefitinika juu ya nafsi yake; basi ufalme wake utasimamaje?[27]Na mimi nikitoa pepo kwa*

*Beelzebuli, je! Wana wenu huwatoa kwa nani? Kwa sababu hiyo hao ndio watakaowahukumu.*

Hii ni sawa na kusema.. walikufuru kwa kudhani ya kuwa YESU ANATOA PEPO KWA NGUVU ZA MKUU WA PEPO kitu ambacho hakikuwa na ukweli wowote. Yesu alikuwa anatoa mapepo kwa nguvu za Mungu.

Angalia na hapa.. **Matendo ya Mitume 10:38** *[38]habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye.*

Nguvu za Roho Mtakatifu...

Nguvu za Mungu

Uwepo wa Mungu ni sababu ya utendaji wa kazi zote njema.

Hii ni kuonyesha kuwa Mungu siyo chanzo cha yale mabaya ila nguvu za Mungu zilitumika kuondoa ubaya.

Wao wakaziita nguvu za mkuu wa PEPO.

Na Yesu alielezea vizuri pale pale **Mathayo 12:28-29**

*[28]Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia. [29]Ama awezaje mtu kuingia ndani ya nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuviteka vyombo vyake, asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu? Ndipo atakapoiteka nyumba yake.*

Kwa hiyo miujiza ya Yesu ni uthibitisho wa utendaji kazi wa nguvu za Mungu na si za shetani. Hivyo kazi ya Mungu waliita ni ya shetani.

Ieleweke kwamba mambo yote aliyoyafanya Yesu na kuyasema yalikuwa na tafsiri katika ufufuo wake.

Angalia.. **Luka 24:44** *[44]Kisha akawaambia, HAYO NDIYO MANENO YANGU NILIYOWAAMBIA NILIPOKUWA NIKALI PAMOJA NANYI, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.*

Maneno na miujiza yake pia.. angalia **Yohana 20:30-31**

*[30]Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. [31]Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake.*

Maneno... miujiza aliyoyafanya YESU YALIKUWA NI ISHARA ... Yanaaelekeza watu kuamini juu ya kufa na KUFUFUKA kwake ili wapate ONDOLEO la dhambi au uzima wa MILELE au kukaliwa na Roho Mtakatifu.

Angalia tena.. Petro anaeleza lengo la matukio aliyoyafanya Yesu Kristo. **Matendo ya Mitume 2:22**

*[22]Enyi waume wa Israeli, sikilizeni maneno haya: Yesu wa Nazareti, mtu ALIYEDHIHIRISHWA KWENU na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara, ambazo Mungu*

*alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua.*

ALIYEDHIHIRISHWA KWENU na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara...

Lengo la miujiza siyi miujiza ila kumdhihirisha Yesu kama MWOKOZI.

Angalia Yesu alivyofanya MUUJIZA wa mikate na samaki na jinsi alivyotumia kama ishara.. kesho yake walimfuata Yesu akawambia WAMWAMINI YEYE wakakataa.. **Yohana 6:27,35-36**

*[27]Msikitendee kazi chakula chenye kuharibika, bali chakula kidumucho hata uzima wa milele; ambacho Mwana wa Adamu atawapa, kwa sababu huyo ndiye aliyetiwa muhuri na Baba, yaani, Mungu.*

*[35]Yesu akawaambia, Mimi ndimi chakula cha uzima; yeye ajaye kwangu hataona njaa kabisa, naye aniaminiye hataona kiu kamwe. [36]Lakini naliwaambia ya kwamba mmeniona wala hamwamini.*

Yesu alipomponya yule kipofu kwenye Yohana 9... baadaye alimfuata AMWAMINI YEYE..

**Yohana 9:1,6,35** *[1]Hata alipokuwa akipita alimwona mtu, kipofu tangu kuzaliwa.*

*[6]Alipokwisha kusema hayo, alitema mate chini, akafanya tope kwa yale mate. Akampaka kipofu tope za macho,*

*[35]Yesu akasikia kwamba wamemtoa nje; naye alipomwona alisema, WEWE WAMWAMINI MWANA WA MUNGU?*

Mpaka hapa tunao ushahidi huu... kuwa..

1. Mambo aliyoyatenda Yesu kwenye vitabu vinne vya Injili yanaelezewa au kutimizwa katika ufufuo wake. Ni kama unabii.

2. Miujiza yote ya Yesu yalikuwa yanaelezea Yeye ni nani na kwamba WAMWAMINI Yeye.. KUMWAMINI Yeye ni kuamini kazi aliyokuwa anatakiwa kufanya katika KUFA NA KUFUFUKA KWAKE.

Hii ina maana kuidharau au kuipindisha miujiza ya Yesu ni kupindisha lengo lake lengo lake ni kuelezea kazi ya Mungu katika Kristo ambao utimilifu wake ni katika ufufuo wake.

Ndiyo maana Yesu aliwakataza wanafunzi wake wasielezee kwanza miujiza yake na maono mpaka atakapofufuka.

Angalia hapa.. **Mathayo 17:1,3,9** *[1]Na baada ya siku sita Yesu akawatwaa Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye, akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani;*

*[3]Na tazama, wakatokewa na Musa na Eliya, wakizungumza naye.*

*[9]Na walipokuwa wakishuka mlimani, Yesu aliwaagiza, akasema, Msimwambie mtu ye yote habari ya maono hayo, hata Mwana wa Adamu atakapofufuka katika wafu.*

Aliwakataza wasiseme hata atakapofufuka...

Maono, miujiza ni ishara zilizokuwa zinawaelekeza watu WAMWAMINI MWOKOZI.

KWANI ROHO MTAKATIFU YEYE ANA UJUMBE GANI?

Angalia Yesu anavyomwelezea Roho Mtakatifu...

Angalia... **Yohana 14:26** *[26]Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.*

Atawafundisha na kuwakumbusha yotr niliyowaambia.

Hapa alikuwa anazungumza habari za ufufuo wake.

Kwa sababu **Luka 24:44** *[44]Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.*

Hii ndiyo kazi aliyosema atawakumbusha.

Yesu alipokuwa anataja habari za Roho Mtakatifu alikuwa anataja habari za Kufa na KUFUFUKA kwake au kutukuzwa kwake.

Hii habari ni muhimu kwa sababu hapo ndipo kulipo na ONDOLEO LA DHAMBI au msamaha wa dhambi.

Angalia.. **Luka 24:44, 46-47** *[44]Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.*

*[46]Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; [47]na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya TOBA NA ONDOLEO LA DHAMBI, kuanza tangu Yerusalemu.*

Kwa jina lake maana yake kwa kile alichokifanya.. Kufa na KUFUFUKA.

Angalia pia.. **Matendo ya Mitume 5:31**

*[31]Mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume, awe Mkuu na Mwokozi, awape Waisraeli toba na msamaha wa dhambi.*

Angalia.. Toba na msamaha wa dhambi.

Toba na ONDOLEO la dhambi.

Toba ni kugeuka.. ili wapate ONDOLEO au Msamaha wa DHAMBI.

Angalia tena.. **Matendo ya Mitume 11:18** *[18]Waliposikia maneno haya wakanyamaza,*

*wakamtukuza Mungu, wakisema, Basi, Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima.*

Ukiangalia Yohana ametumia zaidi UZIMA ... Petro ONDOLEO LA DHAMBI.. Vyote kwa pamoja ni WOKOVU.

**Matendo ya Mitume 4:12** *[12]Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*

Petro hapa ametumia WOKOVU KWA IMANI KATIKA JINA (KAZI KAMILIFU YA YESU KRISTO)..

Tunaweza kusemaje hapa?

Kudharau miujiza ya Yesu Kristo ni kudharau ujumbe uliobebea kule ambapo ni kukataa KUMWAMINI au kuamini katika kufa na KUFUFUKA kwake hivyo kukosa matokeo ya kazi hiyo yaani ONDOLEO LA DHAMBI au MSAMAHA wa DHAMBI.

Hakuna namna unaweza KUSAMEHEWA dhambi bila kuamini.

Kukufuru ni KUTOKUAMINI.

MWAMINI Hawezi kukufuru kwa maana hii.

# SURA YA 4

## *KWA HIYO HAIWEZI KUSAMEHEWA?*

Turudi tena kwenye **Marko 3:28-29** *Amin, nawaambia, Dhambi zote watasamehewa wanadamu, na kufuru zao watakazokufuru zote; 29 bali mtu atakayemkufuru Roho Mtakatifu hana msamaha hata milele; ila atakuwa ana dhambi ya milele,*

Katika andiko hilo hapo juu, alihusisha dhambi ya milele na kukufuru.

Kwa kutumia kanuni ya kutajwa kwa mara ya kwanza, mara ya kwanza kabisa tunaona "kufuru dhidi ya Roho Mtakatifu" iko katika injili ya Mathayo.

**Mathayo 12:31** *Kwa sababu hiyo nawaambia, Kila dhambi na kila neno la kufuru watasamehewa wanadamu, ila kwa kumkufuru Roho hawatasamehewa. [32] Naye mtu ye yote atakayenena neno juu ya Mwana wa Adamu atasamehewa, bali yeye atakayenena neno juu ya Roho Mtakatifu hatasamehewa katika ulimwengu wa sasa, wala katika ule ujao.*

Yesu anazungumza juu ya kufuru dhidi ya Roho Mtakatifu na anasema "*hatasamehewa*".

Katika mstari wa 32b, Yesu anaeleza alichomaanisha kwa kukufuru… **ni kuongea kinyume kwa habari ya Roho Mtakatifu.** Kwa hiyo, **kufuru** ni kusema kinyume.

**Swali ni; Yesu alikuwa anazungumzia nini?**

Katika muktadha, Mistari ya 36 na 37 inatupa mwongozo katika kile ambacho Yesu alikuwa anazungumzia.

**Mathayo 12:36** *Basi, nawaambia, Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu. [37] Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa.*

Pia, alimaanisha nini kwa "***kuhesabiwa haki, na kuhukumiwa*"** kwa maneno yako?

Paulo anatusaidia katika **1 Wakorintho 12** na **Warumi 10**.

**Warumi 10:9** *[9] Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. [10] Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu..*

**1 Wakorintho 12:3** *Kwa hiyo nawaarifu, ya kwamba hakuna mtu anenaye katika Roho wa Mungu, kusema,*

*Yesu amelaaniwa; wala hawezi mtu kusema, Yesu ni Bwana, isipokuwa* ***katika Roho Mtakatifu****.*

Neno *"**kusema**"* ni neno la Kigiriki "**lego**"; ina maana ya kusema kutoka kwa mfumo wako wa imani; wazo.

Neno "***anenaye***" lilitafsiriwa kutoka kwa neno la Kigiriki "**laleo**"; inamaanisha kuzungumza mara kwa mara au mazungumzo ya kawaida.

Neno " ***amelaaniwa***" lilitafsiriwa kutoka kwa neno la Kigiriki "**anathema**"; ina maana ya ***kutenganisha****; kitu ambacho kitakufa; kuiita kuwa kimepotea; kuhukumu kuwa kimekufa*.

Ilikuwa ni neno lile lile lililotumika katika maandiko yafuatayo:

**Warumi 9:3** *Kwa maana ningeweza kuomba mimi mwenyewe* ***niharimishwe na kutengwa*** *na Kristo kwa ajili ya ndugu zangu, jamaa zangu kwa jinsi ya mwili;*

**1 Wakorintho 16:22** *Mtu awaye yote asiyempenda Bwana, na* ***awe amelaaniwa****. Maran atha.*

**Wagalatia 1:8-9** *Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri,* ***na alaaniwe.*** *[9] Kama tulivyotangulia kusema, na sasa, nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea,* ***na alaaniwe****.*

**Kwa hiyo, kukiri huko, yaani, kukiri kufufuka kwa Yesu (Warumi 10:9-10) baada ya mtu kusikia injili ni kwa Roho Mtakatifu. Huu ni wokovu!**

Baada ya kuthibitisha yaliyotangulia, tazama maneno ya Yesu kuhusu huduma ya Roho Mtakatifu.

**Yohana 16:8-14** *[8] Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu. [9] Kwa habari ya dhambi, kwa sababu hawaniamini mimi; 10 kwa habari ya haki, kwa sababu mimi naenda zangu kwa Baba, wala hamnioni tena; [11] kwa habari ya hukumu, kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa. [12] Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa. [13] Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. [14] Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari.*

Atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi.

## <u>Dhambi gani?</u>

**Yohana 1:29** *Siku ya pili yake amwona Yesu anakuja kwake, akasema, Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!.*

Analeta ushahidi wa kifo cha Yesu kwa ulimwengu/mdhambi ili mwenye dhambi aweze kushawishiwa na kuamini.

Ni dhahiri kwamba "kumkufuru" au "kufuru dhidi ya Roho Mtakatifu" itakuwa kukataa (kusema kinyume na) kazi ya ukombozi ya Yesu.

Angalia: **Yohana 16:9**… *Kwa habari ya dhambi, kwa sababu hawaniamini mimi.*

Kwa hivyo, kukufuru kutakuwa ni kupinga huduma ya Roho kwa kutokuamini. Ni kukataa Injili! Ni kusema dhidi ya Kristo, ambaye ni ujumbe wa Roho Mtakatifu.

Baada ya kuona kile ambacho Yesu alikuwa anazungumzia katika Mathayo 12 (Kumkufuru Roho Mtakatifu), swali linalofuata litakuwa:

**Je! Mwanadamu atapata "hukumu" kwa sababu ya kufuru?**

Acheni tuchunguze neno "**kufuru**" kutoka katika vitabu vya Biblia.

Neno "kufuru" lilitafsiriwa kutoka kwa neno la Kigiriki "**blasphemos**"; inamaanisha ***kusema maovu (matusi).*** Ni kuwatendea kwa dharau na kusema maneno kinyume chake. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya mahali ilipotumika: **Mathayo 26:65** *Ndipo Kuhani Mkuu akararua mavazi yake, akisema,* ***Amekufuru****; mna haja*

*gani tena ya mashahidi? Tazameni, sasa mmesikia hiyo **kufuru** yake;*

**Marko 14:64** *Mmesikia **kufuru** yake; mwaonaje ninyi? Wote wakamhukumu kuwa imempasa kuuawa.*

**Yohana 10:33** *Wayahudi wakamjibu, Kwa ajili ya kazi njema hatukupigi kwa mawe; bali kwa **kukufuru**, na kwa sababu wewe uliye mwanadamu wajifanya mwenyewe u Mungu..*

Angalia; katika maandiko hapo juu, Yesu alishtakiwa kwa kukufuru.

**<u>Kwa nini iko hivi?</u>**

## … *Amesema kufuru…*

Angalia **Mathayo 26:63** Lakini, Yesu akanyamaza. Kuhani Mkuu akamwambia, **Nakuapisha kwa Mungu aliye hai, utuambie kama wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu.**

Alitakiwa **<u>aseme</u>…**

Kwa sababu ya kile Yesu alisema… mstari wa 64: “Yesu akamwambia, **<u>Wewe umesema</u>**; maana yake Yesu amekubali kuwa ni mwana wa Mungu. Kwao ni kusema vibaya kuhusu Mungu. Wakasema **mmesikia kufuru yake?**

Kwa hiyo kufuru ni kwa njia ya maneno**; katika kile kinachosemwa!**

Sasa, turudi kwenye Marko 3

**Marko 3:28-29** *Amin, nawaambia, Dhambi zote watasamehewa wanadamu, na kufuru zao watakazokufuru zote; [29] bali mtu atakayemkufuru Roho Mtakatifu hana msamaha hata milele; ila atakuwa ana dhambi ya milele,*

Mstari wa 29 KJV **Mark 3:29** But he that shall blaspheme against the Holy Ghost hath never forgiveness, but is in **danger of eternal damnation:**

**(**SUV wameacha neno **danger)** tutaliangalia baadaye.

Neno "**dhambi**" lilitafsiriwa kutoka kwa neno la Kigiriki "**harmatano**". Ni dhambi mahususi, siyo dhambi zote zilizoko ulimwenguni. Ni neno lile lile lililotumika katika **1 Wakorintho 6:18** … kila dhambi…

Angalia **1 Wakorintho 6:*18*** *Ikimbieni zinaa.* ***Kila dhambi*** *aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake; ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe.*

Kwa hiyo dhambi inaweza kuwa mahususi (specific). Kumbuka kwamba neno "milele" lilitafsiriwa kutoka kwa neno la Kigiriki "**aion/aionios**". Kama inavyoonekana hapo awali, inamaanisha kitu kisichokoma (kisichokoma, kinachoendelea).

Neno "**danger**" lilitafsiriwa kutoka kwa neno la Kigiriki "**enochos**"; ina maana ya *kuwa na hatia, kuwajibika*.

**Kwa hiyo, kile ambacho Yesu alikuwa akisema ni kuwa na hatia ya kuendelea kufanya dhambi! Kwa hiyo, Yesu alikuwa anazungumza juu ya mtu ambaye anaendelea kusema mabaya dhidi ya Roho Mtakatifu.**

**Vipi kuhusu Paulo, aliyejiita mkufuru?**

**1 Timotheo 1:12-13** *Nami namshukuru Kristo Yesu Bwana wetu, aliyenitia nguvu kwa sababu aliniona kuwa mwaminifu, akaniweka katika utumishi wake; [13] ingawa hapo kwanza nalikuwa* ***mtukanaji****, mwenye kuudhi watu, mwenye jeuri, lakini nalipata rehema kwa kuwa nalitenda hivyo kwa ujinga, na kwa kutokuwa na imani.*

Neno la Kiswahili ***mtukanaji*** ni lile lile neno la Kigiriki **blasphēmos.** Paulo anasema naye alikwa mtukanaji au mtu anayekufuru. Aliwaudhi watu (injurious). Ina maana Paulo alitukana mambo ya Roho Mtakatifu wakati akina Stefano walipokuwa wanahubiri. Aliyasema vibaya na kuyadharau na ndiyo maana alikuwa anaendelea mbele kwenda kuwaangamiza. Ni kweli alikufuru. [13]***Who was before a blasphemer, and a persecutor, and injurious: but I obtained mercy, because I did it ignorantly in unbelief.*** Aliwadhuru watu, hata hivyo, alipokea msamaha. Anasema "**nalitenda hivyo kwa ujinga, na kwa kutokuwa na imani**".

**Kwa hiyo, Paulo hatakuwa na hatia ya kukufuru kwa sababu hakuendelea nayo. Aliamini injili. Amepata rehema.**

Tena, turudi Marko 3.

**Marko 3:28-29** *Amin, nawaambia, Dhambi zote watasamehewa wanadamu, na kufuru zao watakazokufuru zote; [29] bali mtu atakayemkufuru Roho Mtakatifu hana msamaha hata milele; ila atakuwa ana dhambi ya milele;*

Kwa hiyo, watu kama hao wanakana Ubwana wa Yesu, ufufuo wake, msamaha katika damu yake na wanachukulia dhabihu yake kwa ajili ya dhambi kama **upuuzi**.

**Kwa hiyo, mtu anayekufuru hajaokoka.**

**Yesu alikufa ili kutoa wokovu kwa wote na yeyote anayekataa wokovu huo kwa kutokuamini katika injili ya Kristo ni mwana wa uasi, na atakabiliwa na adhabu itakayowapata wana wa uasi.**

Kwa hivyo, inatosha kusema kwamba kumkufuru Roho Mtakatifu si tendo la mara moja bali ni la kuendelea. Wakati mtu (kama vile Paulo katika 1 st Timotheo 1:12-13) anaamini, anapokea rehema ya Mungu/wokovu na ameepuka ghadhabu inayokuja. Kukufuru mwisho wake ni kuamini. Asipoamini anabaki kuwa mtu wa makufuru, asiyeamini na hukumu ya milele.

## Vitabu Vingine Vya Shemeji Melayeki

## KISWAHILI

1. *Ukombozi Reloaded*
2. *Kufunga Reloaded*
3. *Moyo wa Baba*
4. *Akaanza Kutoka Musa I*
5. *Yanipasa Nifanye Nini Nipate Kuondoka?*
6. *Uinjilisti na Uanafunzi*
7. *MAOMBI: Bwana Tufundishe Sisi Kusali*
8. *Chapa Ya Kudumu*
9. *Msimzimishe Roho*
10. *Akaanza Kutoka Musa II*
11. *Kwa Kuwa Sasa Nimeokoka!*
12. *UFUATILIAJI*
13. *Nataka Kumwona Yesu – Kijitabu cha 1-4 (watoto)*
14. *Niko Tayari kwa Ndoa?*
15. *KUHUSU KUUNGAMA DHAMBI*
16. *MSIPOWASAMEHE WENGINE*
17. *KUMKUFURU ROHO MTAKATIFU*

## ENGLISH

1. *Evangelism and Discipleship*
2. *Believer's Eternal Seal*
3. *Now, That I am Born Again!*
4. *Seeing Jesus Christ Book 1-4 (Children's Book)*

# KUHUSU SISI

Huduma ya Global Family Gatherings imejikita katika kufundisha Neno la Mungu kwa uchambuzi wa Maandiko hatua kwa hatua. Nia yetu hasa ni kuishi katika mpango wa Mungu wa kwenda kuhubiri Injili na kutengeneza wanafunzi. Mwisho wa siku tuhakikisha kila mtu, kila mahali amefikiwa na kuimarisha katika kweli ili awe mtu imara na mwenye kutimiza mapenzi ya Mungu hapa duniani.

**Mafundisho kwa njia ya audio**
https://globalfamilygatherings.co.tz/messages/
**Vitabu vyetu nakala tete**
https://globalfamilygatherings.co.tz/our-books/
Makusanyiko simu +255 714 548 565 au
https://globalfamilygatherings.co.tz/about/ utaona maeneo yote yenye makanisa yetu.
Telegram: https://t.me/apostleshemeji
Youtube channel:
https://youtube.com/c/shemejimelayeki
Facebook page: https://facebook.com/ShemejiMelayeki